

HALMASHAURI YA WILAYA YA KONDOA

MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA MANUNUZI KILICHOFANYIKA TAREHE 25.10.2021

WALIOHUDHURIA

| | | |
|----------------------|-------------------------------|------------|
| • Magreth Temu | Afisa Elimu Msingi (W) | Mwenyekiti |
| • Samwel Mseselo | Afisa Manunuzi (W) | Katibu |
| • Juvenal Munishi | Afisa Kilimo (W) | Mjumbe |
| • Archanus kilaja | Afisa utumishi na Utawala (W) | Mjumbe |
| • Mashauri M Vicent | Mwanasheria (W) | Mjumbe |
| • Dr Christian Mwiga | Afisa Mifugo (W) | Mjumbe |
| • Dr Nelson Kimolo | Mganga Mkuu(W) | Mjumbe |

Waalikwa/wasa

- Isack Lwambano Mratibu LDFS

MUHT.05/10/TB/2021/2022-KUFUNGUA KIKAO

Katibu wa Bodi ya Zabuni alimkaribisha Mwenyeki kufungua kikao ambapo mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe katika kikao na kuwaomba michango yao ya hali na mali katika kupitia taarifa za manunuzi. Mwenyekiti alifungua kikao saa 08:25 Asubui.

MUHT.06/10/TB/2021/2022 KUTHIBITISHA AGENDA ZA KIKAO

Wajumbe wa bodi ya zabuni walipitisha agenda zifuatazo kuwa ndio agenda za kikao

- Kufungua Kikao.
- Kuridhia agenda.
- Kupitia muhtasari wa kikao kilichopita cha tarehe 05.07.2021
- Kupitia manunuzi mbalimbali yaliyopitishwa kwa njia ya waraka
- Kuridhia njia ya ununuzi kwa ajili ya miradi ya Covid 19, uchimbaji wa visima na kitabu cha zabuni kwa ajili ya uchimbaji wa visima mradi wa LDFS.
- Mengineyo
- Kufunga Kikao

**MUHT NA MUHT.09/10/TB/2021/2022 KURIDHIA NJIA YA UNUNUZI NA
KITABU CHA ZABUNI.**

**• KUPITIA KITABU CHA ZABUNI NA NJIA YA UNUNUZI KWA AJILI YA
MRADI WA LDFS**

Katibu wa bodi ya zabuni aliwasilisha taarifa ya kuwa ktumepokea fedha kwa ajili ya uchimbaji wa visima nane Haubi na mafia ambapo mradi huu niwaufadhili.Kutokana na maelekezo ya mradi huu ni kuwa unatakiwa kutekelezwa kabla kipindi cha mvua hakijaanza,hivyo kitengo cha manunuzi kinapendekeza tutumie njia ya Restricted Tendering kama ilivyoainishwa kwenye kanuni ya ununuzi wa umma,kanuni ya 152 ya mwaka 2013 na marekebisho yake ya mwaka 2016 kutokana na utumiaji wa njia hii kuwa mfupi ukilinganishwa na njia nyingine za ununuzi.

Pia katibu aliwasilisha kitabu za zabuni kwa ajili ya kupata ridhaa ya bodi ya zabuni kuwa punde tutakapopata kibali cha kuendelea na kazi hii taratibu ziendelee, kama ilivyoainishwa kwenye kanuni namba 185 ya kanuni za manunuzi ya umma ya mwaka 2013 ikisomwa pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2016.

Baada ya maelezo hapo juu ya katibu wajumbe wa bodi ya zabuni waliridhia kutumia njia ya restricted tendering na kitabu cha zabuni kwa ajili ya uchimbaji wa visima nane haubi na mafai

**• KURIDHIA NJIA YA UNUNUZI KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MIRADI
YA COVID-19**

Katibu pia aliwaeleza wajumbe wa bodi ya zabuni kuwa Halmashauri imepokea fedha za IMF kwa ajili utekelezaji wa miradi ya shule na afya na ambapo fedha hizi tumepewa tuzitekelezae kwa kipindi cha mwezi mmoja,kulingana na mazingira ya utekelezaji wa shughuli hizi za ujenzi wa miundombinu hii ya madarasa ya sekondari na nyumba ya watumishi wa afya tunaomba bodi yako iridhie kutumia njia ya Force Account kama ilivyoainishwa kwenye Kanunuzi za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013 kanuni ya 167 ikisomwa pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2013.

Baada ya maelezo ya katibu wa zabuni hapo juu wajumbe wa Bodii ya zabuni waliridhiiia itumike njia ya Force Account kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya covid19 kama kanuni za manunuzi zinavyoolekeza

MUHT NA MUHT.09/10/TB/2021/2022 MENGINEYO

Wajumbe wa bodi ya zabuni walishauri mambo yafuatayo yafanyike kwa ajili ya maslahi mapana na Halmashauri na kuwepo na kumbukumbu mzuri za manunuzi ambapo mambo yenye ni

- Katibu kuwaelekeza bodi ya zabuni kuhusu sharia na taratibu za manunuzi kwa manunuzi yote yanayofanyika.
- Kwa kazi ambazo sio za haraka sana bodi inaomba tufanye vikoa kuliko kuitisha manunuzi hayo kwa njia ya waraka.
- Kuongezeke umakini katika kamati za mapokezi ya vifaa mbalimbali vinavyonunuliwa na Halmashauri hasahasa katika miradi ya ujenzi na kamati za mapokezi ziandike taarifa za mapokezi ya vifaa punde vinapopokelewa.

MUHT NA MUHT.10/10/TB/2021/2022 KUFUNGA KIKAO

Katibu wa Bodi ya zabuni alimkaribisha mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango yao na kuendelea kukazia kuwa ushauri walioutoa uzingatiwe.Kikao kilifungwa saa 09:30 asubui

MUHTASARI UMETHIBITISHWA

KATIBU

MWENYEKIT